## HABARI KITAIFA



Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, akizungumza na wataalamu mkoani Tanga jana, kabla ya kikao kazi cha kujadili mikakati na kampeni ya kuhamasisha shughuli za ukuzaji viumbe maji baharini. Kulia kwake ni Mkuu wa Wilaya ya Tanga, Hashim Mgandilwa. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA**

# Kesi kupinga kujiuzulu

Scanned with CamScanner

# Ufugaji wa samaki kwa vizimba kuwaneemesha vijana Mwanza

Na Nashon Kennedy

FAIDA mojawapo ya mtu kula samaki ni pamoja na kupata virutubisho muhimu kwenye mwili wake kama vile vitamini D na B2, kuongeza kiwango cha madini ya chuma.

Mratibu wa Lishe Mkoa wa Mwanza, Sophia Lugome anasema lishe bora ni mchanganyiko wa makundi matano ya chakula, ambayo kila binadamu anatakiwa kula kwa ajili ya kuwa na afya bora na kujikinga na maradhi mbalimbali.

Anayataja makundi hayo ya chakula kuwa ni vyakula vya nafaka, mizizi na ndizi mbichi, vyenye asili ya wanyama, wadudu na jamii ya mikunde kunde, mbogamboga, matunda, mafuta, sukari na asali.

Lugome anasisitiza kuwa ulaji wa samaki ni muhimu kwa sababu ni miongoni mwa chakula kilichopo katika kundi la vyakula vyenye asili ya wanyama, wadudu na jamii ya mikunde kunde.

"Kundi hili ukitumia unapata utomwili (protini)," anasema na kuongeza kwamba kundi hilo limegawanyika katika makundi mawili, daraja la kwanza kwa mtu anayetumia vyakula vyenye asili ya wanyama na wadudu na daraja la pili kwa mtu anayetumia vyakula vyenye asili ya mikundekunde," anasema.



Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Robert Gabriel.



Ufugaji samaki wa vizimba.

### FAIDA SAMAKI

Lugome anasema umuhimu wa kula samaki na virutubisho vinavyopatikana katika samaki ni muhimu kwa madai kuwa samaki ni miongoni mwa chakula kilichopo katika kundi la vyakula vyenye asili ya wanyama, wadudu na jamii ya mikunde kunde.

Anasema virutubisho vinavyopatikana katika samaki, endapo mtu ataitumia kama lishe kuwa ni pamoja na omega-3, vitamini D na B12 (Riboflavin) na madini ya chuma (iron), zinki, joto (iodine), magnesia (magnesium), kalisi (calcium) na potasiamu.

Anasema kundi hilo limegawanyika katika makundi mawili ya daraja la kwanza, mtu akitumia vyakula vyenye asili ya wanyama na wadudu na daraja la pili kwa atakayetumia vyakula vyenye asili ya mikundekunde.

Anasema madini ya potasiamu yanasaidia katika kuimarisha utendaji kazi wa misuli ya moyo, omega -3 inasaidia katika kuimarisha uono wa macho na ukuaji wa ubongo na kuwa na ufahamu wa hali ya juu na utunzaji wa kumbukumbu.

Anaongeza kuwa madini ya kalisi yanasaidia kuimarisha ukuaji wa mifupa na kuifanya iwe imara, madini ya chuma yanaongeza wingi wa damu, madini joto yanawaepusha watu kutopata tatizo la goita hivyo kutumia samaki kunaleta faida nyingi mwilini pamoja na kutengeneza seli zilizoharibika, kuimarisha ukuaji mzuri wa mwili na kuufanya usiwe na uzito uliozidi.

"Tafiti zinaonesha mtu anayetumia samaki mara kwa mara anakuwa na uwezekano mdogo wa kupata maradhi ya moyo kama kiarusi au kupoteza maisha kwa ajili ya magonjwa ya moyo," anasema Lugome.

Anasema inashauriwa mtu kula samaki mara mbili kwa wiki au kila siku kwani hakuna madhara kuliko kula nyama nyekundu hasa nyama ya ng'ombe na mbuzi na kiasi cha samaki kinachohitajika ni robo ya samaki kwa mlo kwa siku ila inategemea na umri wa mtu.

Ni kwa mantiki hiyo, kwa kuthamini umuhimu wa lishe inayotokana na samaki, Mkoa wa Mwanza umeanzisha mkakati wa kupunguza umaskini na kukuza uchumi kupitia sekta ya uvuvi kama ilivyobainishwa wazi katika Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa miaka mitano (2021-2025).

Mkakati huo unalenga katika kuiwezesha jamii kutumia rasilimali za mazao ya samaki yaliyo katika ziwa hilo kwa shughuli za kiuchumi, kujiajiri na kupata lishe bora.

Hii ni kwa sababu mazao ya uvuvi yaliyo katika Ziwa Victoria ni miongoni mwa sekta muhimu inayochangia kuondoa umaskini na kukuza uchumi wa Mkoa wa Mwanza na taifa kwa ujumla.

Pamoja na kuwepo kwa fursa hizo katika ziwa, eneo hilo bado halijapewa msukumo wa kutosha ili kutimiza lengo hilo licha ya fursa zilizopo.

Kwa mujibu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu ya Taifa, sekta hiyo ya uvuvi inachangia asilimia saba ya pato la mkoa na 1.7 ya pato ghafi la taifa (GDP), ambapo sekta nzima ya uvuvi inachangia asilimia 10 ya mauzo nje ya nchi.



ya samaki kwa vizimba.



Katibu Tawala Msaidizi (Idara ya Uchumi na Uzalishaji), Emil Kasagara.

Kwa kutambua fursa zilizopo katika Mkoa wa Mwanza, mkoa huo umeandaa "Mkakati wa kukuza uzalishaji endelevu wa samaki kwa njia za kisasa".

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Robert Gabriel anasema mpango huo umelenga katika kuwezesha vikundi vya vijana na kuhamasisha vyama vya ushirika, kampuni na watu binafsi kufanya ufugaji wa samaki wa kisasa kwa kutumia vizimba.

Anasema ufugaji wa samaki kwa njia ya vizimba katika Ziwa Victoria umeongezea kwa kasi mkoani Mwanza, ikichangiwa zaidi na kuongezeka kwa hamasa ya ufugaji huo na hivyo kusababisha kupungua kwa rasilimali ya uvuvi kutoka vyanzo vya asili.

### WALENGWA WA MKAKATI

Gabriel anasema vizimba vya kufugia samaki vilivyo ndani ya ziwa kwa takwimu za hivi karibuni ni 362 kati ya vizimba 473 vilivyoko nchini.

Anasema Mkoa wa Mwanza pekee una vizimba 309, ambapo jumla ya wawekezaji 28 ndio wanaojishughulisha na ufugaji wa aina hiyo ya samaki katika wilaya za Nyamagana, Magu, Sengerema, Buchosa na Ukerewe.

"Lengo ni kuwawezesha vijana wetu kufuga samaki kwa njia ya vizimba ili waweze kujiajiri na kujikomboa kiuchumi," anasema mkuu huyo wa mkoa.

Anasema mpango huo pia utawahamasisha wananchi wa mkoa huo na wa nje kupitia kwa maofisa uvuvi na wataalamu wa kada tofauti za mazao ya samaki hasa wale waliojiunga na kuanzisha vyama vya ushirika, wachakataji, wasindikaji na wafanyabiashara wa mazao ya uvuvi, vikundi vya wajasiriamali na kijamii na taasisi binafsi zenye dhamira ya kuwekeza katika ufugaji wa samaki kwa njia ya vizimba na kufanya uwekezaji huo.

Katibu Tawala Msaidizi (Idara ya Uchumi na Uzalishaji), Emil Kasagara, anasema mkoa una vikundi vya vijana 64 ambavyo vimeonesha nia ya kufuga samaki kwenye vizimba vyenye zaidi ya wanachama 640 na vyama vya ushirika wa wavuvi 21 vyenye jumla ya wanachama 556.

Kasagara anasema kwa kuanzia mkoa umepanga kuanza na vikundi vya vijana 35 kutoka katika halmashauri saba zinazopakana na Ziwa Victoria.

Anasema hadi sasa vyama 12 kati ya 21 vilivyopo mkoani Mwanza vimeonesha dhamira ya kuanza ufugaji wa samaki kwenye vizimba, ambapo tayari vimeandaa na kuwasilisha maandiko ya mradi katika Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania kuomba mikopo ili kufanikisha kazi hiyo.

Anasema mkoa kwa kushirikiana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi kupitia Wakala wa Mafunzo ya Uvuvi (FETA) wametoa mafunzo ya ufugaji wa samaki kwenye vizimba kwa vikundi vyote vyenye nia ya kufa samaki kwa vizimba.

Anasema vijana 195 kutoka vikundi 44 wamepatiwa mafunzo wakiwemo wajumbe wa vyama vya ushirika 58 na watu binafsi 10 wameshiriki kwenye mafunzo hayo.

Vijana hao watawezeshwa kuingia kwenye mpango huo wa ufugaji yakiwemo mahitaji muhimu (vizimba, chakula cha samaki na vifaranga vya samaki) kupitia kwenye asilimia nne ya mikopo inayotokana na mapato ya halmashauri ili wajikomboe kiuchumi.

Scanned with CamScanner

our com-
munities
bank be
r said.
Commis-
ge com-
or being
lping the
ing them
ould be

support
e people
he health
upon by
ra ward
s.
ati Town
Abdlura-
support
that the
r healthy

division
ed to us.
of Babati
iness and
rowed all
ave done
the busi-
ople.
he area
ent. Asia
ompletion
saka cen-
ve health
wards and

into a humped stance.

Financial experts ex-

curve has slightly adjusted downwards at almost the

transactions last week from 4.82 million shares traded.

market review that the equities recorded a good

the secondary market," Masumbuko said.

DAILY NEWS Page 19



*LIVESTOCK and Fisheries Deputy Minister, Abdallah Ulega talks to the fishery experts on the ministry's strategies before opening a strategic working session and a campaign to promote marine aquaculture activities for leaders and experts in Tanga Region yesterday. Taking notes on the left is Tanga District Commissioner, Hashim Mgandilwa and Tanga Regional Economic and Production Department Head Emigidius Kasunzu.(Photo by Tanga Regional Commissioner's office)*

THE ov
declined
the perio
last year
cent rec
ing mon
in the
2020.
The
(BoT)
view f
shows
lending
custom
chang
Ac
port,
depos
Nove
overa
avera
comp
and
Octob
ber 2
M
ed dep
tomers
averag
vember
Dur
riod, the
private se
cover, grow

Scanned with CamScanner

THE GUARDIAN Page 2.



Livestock and Fisheries minister Abdallah Ulega has an audience in Tanga city yesterday with experts with the ministry based in Tanga Region. It was shortly before the start of a meeting on the strategic implementation of activities related to marine aquaculture.